Nabii Aliyependelewa Bila Sababu

Sura ya 6

Somo la Kusikiza: Agano la Kale Namba 79

Shabaha: Kuelewa ujumbe wa upendo wa Mungu katika kitabu cha Yona.

Watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka.

- 1 Petero 3:9

"---- kwa sababu nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya."

- Yona 4:2

Manabii wa Agano la Kale walifuata mtindo fulani katika uhusiano wao na Mungu. Walikuwa na ujuzi wa kumjia Mungu uliokuwa wa maana, na kisha wakawa na ujuzi wa kwenda kwa ajili ya Mungu uliokuwa na matunda. Lakini Yona anatuonyesha mtindo huu kwa kwenda kinyume nyume. Katika sura ya kwanza hakuja kwa Mungu na hakuenda kwa ajili ya Mungu. Kwa sura ya pili hata hivyo anakuja kwa Mungu akisema: 'Nita' mara tatu katika tumbo la samaki. Baada ya kukutana huku na Mungu anaenda Ninawi kwa ajili ya Mungu kwa sura ya 3.

Mada ya msingi ya kitabu cha Yona ni Mungu ni upendo kwa watu wote, hata watu wanaochukiwa kama Washami katika Ninawi walivyokuwa. Ingawa Yona alikuwa anachuki na hasira kuwa Mungu angewasamehe Waninawi. Mungu kwa uvumilivu mwingi alimwoonyesha upendo wake mkuu kwa watu wa mji huu.

1. Ukweli au uongo? Yona alijua kuwa Mungu alikuwa na upendo na nguvu za kuwaongoza watu wa Ninawi.

2. Ukweli au uongo? Mungu mara nyingi hutulazimisha kufanya mapenzi yake.

3. Ukweli au uongo? Katika tumbo la samaki Yona alijitolea kutii mapenzi ya Mungu.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

4. Ni gani kati ya yafuatayo aliyofanya Yona akiwa kwa tumbo la samaki?
(chagua yote yaliyosahihi)
    a. Alimlaumu Mungu kwa shida zake
    b. Alimuuliza Mungu ahukumu watu wa Ninawi kwa dhambi zao
    c. Alinukuu maandiko
    d. Aliimba tenzi
    e. Aliomba
    f. Aliuliza Mungu amwache afe
    g. Aliweka nadhiri ya kumtii Mungu
    i. Alijaribu kuheba na akaogelea hadi akawa salama

5. Kwa nini Mungu mara nyingi anaruhusu watumishi wake washikwe katika hali ngumu?
    a. Kuwafunja moyo
    b. Kuonyesha kuwa hawapendi tena
    c. Kuwafanya wategemee raslimali zao wenyewe
    d. Kupata mwitikio sawa kutoka kwao

6. Mungu huwafanyia nini watumishi wake wanapoitikia kwa usahihi katika hali zao ngumu?
    a. Anawaacha hapo kwa muda mrefu ili kuwafunza somo
    b. Anawaacha wajilipie tena gharama ya kurudi ndani ya kibali chake
    c. Anawaokoa na kuwarejesha
    d. Anafanya mambo yote kuwa rahisi kwao tena

7. Watu wa Ninawi waliitikia vipi Yona alipowaambia habari za kuangamia kwao?
    a. Walitubu dhambi zao na wakaamini
    b. Walimpiga Yona kwa mawe
    c. Walimkimbiza Yona toka kwa mji
    d. Walimpuuza kabisa

8. Mungu aliitikiaje watu wa Ninawi?
    a. Aliharibu mji huo baada ya siku 40
    b. Alituma manabii wengi kwao
    c. Aliwasamehe na kuwaacha wasihukumiwe
    d. Aliwapa uwezo wa kushinda maadui zao wote.

9. Yona alifikiria nini kuhusu toba ya watu wa Ninawi?
    a. Alifurahia na akamsifu Mungu kwa wema wake
    b. Hakuamini kama mwitikio wao ulikuwa usio na unafiki
    c. Alifikiria wangefaa kumshukuru sana yeye
    d. Alimkasirikia Mungu kwa sababu aliwachukia sana watu wa Ninawi

10. Mungu aliitikia vipi hasira ya Yona?
    a. Kwa uvumilivu alimwonyesha Yona mafikira yake kwa ajili ya mji huo
    b. Alimkasirikia Yona na akamrudisha ndani ya tumbo la samaki
    c. Alimwomba Yona radhi na akamtuma arudi Israeli
    d. Aliamua kuangamiza Ninawi baada ya yote.

11. Ni watu wa aina gani ambao Mungu anapenda sana?
    a. Wayahudi
    b. Wahindi
    c. Waamerika
    d. Mungu anapenda watu bila kujali kabila lao au kiwango chao

12. Ni zipi zilizo baadhi ya jumbe muhimu katika kitabu cha Yona? *(chagua zote zilizosahihi)*
    a. Muijiza wa samaki kumeza nabii
    b. Ukatili wa watu wa Ninawi
    c. Hali ya kibinadamu ya kuchukia au kupendelea bila sababu
    d. Upendo wa Mungu

Je, unachuki isyo na sababu? Kuna mtu yeyote uliye na ugumu kumpenda? Kwa nini inakuwa vigumu kuwapenda? Unafikiria Mungu anahisi vipi kuwahusu? Mungu anataka wewe uhisi vipi kuwahusu?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwa sababu yeye ni Upendo na kwamba upendo wake unafikilia dunia nzima. Muulize akupe fursa ya kuwaambia wengine juu ya upendo wake kupitia Yesu Kristo. Ikiwa fursa zingine kama hizo ni ngumu, muulize akupe ujasiri wa kumtii.

KUZAMA ZAIDI

1. Kwa nini Yona aliwachukia watu wa Ninawi sana hivyo? (Fanya uchunguzi juu ya Washami ambao walikuwa maadui wabaya muno, Israeli iliwahi kuwa nao. Haswa chunguza ukatili na matendo ya kinyama waliofanya walipowashinda watu wengine.) _____
_____
_____
_____

2. Kuna umuhumu gani kwa taarifa hii kuwa neno la Bwana likamjia Yona kwa *mara ya pili?*__
_____
_____
_____

3. Tunajifunza nini kuhusu ulinganisho kati ya mapenzi ya hiari ya mwanadamu na mapenzi makuu ya Mungu, vile Yona anaomba na mara tatu anakiri 'nita' katika tumbo la samaki mkubwa? _____
_____
_____
_____

4. Tunajifunza nini kuhusu ni nani aliye wabadilisha watu wa Ninawi kwa njia ambayo Yona aliitikia mwito wa uinjilisti wa krusadi kubwa ambayo dunia imewahi kujua? _____
_____
_____
_____

5. Ni kwa njia gani tunasaidiwa kufafanua maana ya kitabu hiki na matumizi ya ujumbe wa nabii huyu, ikiwa ukweli ni kwamba Yona mwenyewe ndiye aliyekiandika, na hii inamfanya aonekane kama mtu wa msaha? _____
_____
_____
_____

6. Ni kizuizi gani kilichokuwa kinashukulikiwa na Yona alipoandika kitabu hiki? _____
_____
_____
_____

7. Ni kwa njia gani ujumbe wa Yona unahusiana na wewe kibinafsi? _____
_____
_____
_____